

Frelimo yatunisha mfuko wake kwa ngoma za kisasa

Ngurumo 17 April 62

MITINDO mbali mbali ya ngoma za kisasa kama Twist, Chachacha na Samba yalikuwa motomoto mjini Morogoro hivi majuzi, nayo yalikuwa rasmi yakichezwa na akina mama wa Yuth ya Frelimo.

Kiongozi mmoja ambaye anaongoza msafara huo amesema kwamba Yuth hiyo ya Frelimo imo safarini katika Mkoa wa Mashariki kwa madhumuni ya kucheza chachacha ili kuingiza mapesa kwenye mfuko wa Frelimo.

Licha ya kucheza ma-

chachacha, pia jamaa hawa watakuwa wanacheza michezo ya kuigiza. Katika mpango wao wasafiri wanatazamia kuitembelea Kimamba na Ilonga wakifuatana na band ya Cuban Marimba ya Morogoro na hatimaye warejee Dar. kuwaki-lisha walichopata.